

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA**



**HALMASHAURI YA WILAYA YA
NJOMBE**

Kumb Na: NDC/PMU/3/VOL. III/06

Tarehe: 15/06/2023

TANGAZO LA ZABUNI

MWALIKO WA KUPATA ORODHA YA MAFUNDI WA SHUGHULI ZA UJENZI WA MAJENGO MWAKA WA FEDHA 2023/2024 'LOCAL FUNDI'

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anawatangazia wananchi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi za ufundi wa kujenga majengo/nyumba mbalimbali za serikali kujitokeza na kuwasilisha maombi ya kuingia kwenye orodha (short list) ya mafundi kwa miradi itakayotekelezwa kwa kutumia mafundi wa kawaida (Local Fundi) kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024.
2. Mafundi wanaohitajika ni fundi kujenga, uashi, seremala, umeme, chuma (Grill & Welding) na vioo (Aluminium).
3. Dhumuni la mwaliko huu ni kuhakikisha tunapata orodha ya mafundi wenye sifa na uzoefu ambao tutawatumia kwa utaratibu wa ushindani kwenye miradi tunayotarajia kutekeleza kwa utaratibu wa 'Force Account' kwenye maeneo yetu ya Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali, Shule za Msingi/Sekondari na Makao Makuu ya Halmashauri.
4. Shughuli za ujenzi zitahusisha mafundi waliochanganuliwa kwenye jedwali hapa chini na wawe na sifa zinazohusika:-

LOT NAMBA	AINA YA MAFUNDI	SIFA ZINAZOHITAJIKA
LOT 1	Fundi Uashi/Kujenga	<ol style="list-style-type: none">Ajue kusoma ramani na kitafsiriAjue kujenga kwa mawe na tofaliAjue kupiga lipu kuta za mawe na tofali

		<ul style="list-style-type: none"> iv. Ajue kuweka sakafu vizuri na iliyonyooka v. Ajue kuweka malumalu (tiles) vi. Ajue kuseti masinki ya vyoo vii. Ajue kumalizia lipu (skimming) viii. Ajue kutumia Zege ix. Ajue michanganyo ya mota x. Ajue kuchanganya saruji (cement) na mchanga xi. Ajue kuweka tarazo xii. Awe na uzoefu wa kazi na uwezo wa kuthibitisha sehemu alizowahi kufanya xiii. Ajue vifaa vya fundi uashi
LOT 2	Fundi Seremala	<ul style="list-style-type: none"> i. Ajue kusoma ramani ii. Ajue aina za mbao iii. Ajue aina za mabati ya kuezeka iv. Ajue vifaa vya fundi seremala v. Awe na uzoefu wa kazi na uwezo wa kuthibitisha sehemu alizowahi kufanya kazi
LOT 3	Fundi Rangi	<ul style="list-style-type: none"> i. Ajue kuchanganya rangi ii. Ajue matumizi ya rangi iii. Ajue aina za rangi iv. Ajue vifaa vya fundi rangi v. Awe na uzoefu wa kazi na uwezo wa kuthibitisha sehemu alizowahi kufanya kazi ya upakaji wa rangi

